RISALA YA MWENYEKITI WA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI MHE. JAJI (R) SEMISTOCLES KAIJAGE KUHUSU UPIGAJI KURA KATIKA UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE JIMBO LA DIMANI ZANZIBAR NA KATA 19 ZA UDIWANI TANZANIA BARA TAREHE 22 JANUARI, 2017

Ndugu Wananchi;

Kama mnavyofahamu kesho tarehe 22, Januari 2017 ni Siku ya Kupiga kura katika Uchaguzi mdogo wa Mbunge Jimbo la Dimani Zanzibar na Kata 19 za Udiwani Tanzania Bara. Tume ya Taifa ya Uchaguzi, ndicho chombo chenye dhamana Kikatiba Kuratibu, Kusimamia na Kuendesha Chaguzi za Rais, Wabunge na Madiwani.

Awali ya yote nawapongeza wananchi wote wa Jimbo la Dimani Zanzibar na Kata 19 za Udiwani Tanzania Bara kwa utulivu mliouonyesha wakati wa kipindi cha Kampeni za Uchaguzi. Ingawa kulikuwa na dosari za hapa na pale; juhudi zilifanywa na Tume ya

Taifa ya Uchaguzi, kukemea vitendo hivyo ili kuwezesha Kampeni za Uchaguzi kufanyika kwa Usalama na Amani.

Ndugu Wananchi;

Katika Uchaguzi huu mdogo wa Mbunge, jumla ya Wapiga Kura 9,280 wa Jimbo la Dimani Zanzibar wanatarajiwa kupiga kura ili kumchagua Mbunge wao atakayewaongoza. Aidha, kutakuwepo na jumla ya Vituo 29 vya Kupigia Kura katika Jimbo hilo.

Kwa upande wa Uchaguzi Mdogo wa Madiwani katika Kata 19 za Tanzania Bara, Jumla ya Wapiga Kura 134,705 walioandikishwa wanatarajia kupiga kura na kutakuwa na Vituo vya Kupigia Kura 359.

Natoa rai kwa wale wote mliojiandikisha kama Wapiga Kura kujitokeza kwenye Vituo vilivyotumika wakati wa Uchaguzi Mkuu wa 2015 ili kuweza kupiga kura na kuwachagua viongozi mnaowataka bila hofu, woga, wasiwasi au ushawishi. Kura ni haki yako na ni kwa mustakabali wako na nchi yetu.

Ndugu Wananchi;

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inapenda kuwakumbusha Wapiga Kura wote mambo yafuatayo:-

(i) Vituo vitafunguliwa saa 1:00 asubuhi na kufungwa saa 10:00 jioni. Iwapo wakati wa kufunga Kituo watakuwepo Wapiga Kura katika mstari ambao wamefika kabla ya saa kumi jioni na hawajapiga Kura, hao wataruhusiwa Kupiga Kura. Mtu yeyote hataruhusiwa kujiunga katika mstari wa Wapiga Kura baada ya saa kumi (10:00) jioni.

(ii) Mpiga Kura akumbuke kubeba Kadi yake ya Mpiga Kura. Sheria ya Uchaguzi inaelekeza kuwa ili Mpiga Kura aruhusiwe kupiga kura ni lazima awe na kadi ya Mpiga Kura. Fomu Na. 17 sio mbadala wa Kadi ya Mpiga Kura.

(iii) Wapiga Kura ambao wana Kadi ya Mpiga Kura lakini taarifa zao hazimo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Kituoni, **hawataruhusiwa kupiga kura.**

(iv) Ni marufuku, na ni kosa la jinai kumkataza mtu kwenda Kupiga Kura.

(v) Kipaumbele kitatolewa kwa wagonjwa, watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali, wanawake wajawazito au wenye watoto wachanga na wazee ambao hawatatakiwa kujipanga kwenye mstari.

(vi) Wakati wote wa Kupiga Kura na Kuhesabu Kura, Mawakala wa Vyama vya Siasa wawepo kwenye vituo. Wajibu wao ni kulinda maslahi ya Vyama vyao na Wagombea. Hata hivyo, hawatakiwi kuingilia masuala ya utendaji ambayo yamekabidhiwa kwa Msimamizi wa Kituo.

(vii) Kura zitahesabiwa katika Kituo cha Kupigia Kura mara tu Upigaji Kura utakapokamilika. Baada ya Kura kuhesabiwa,

Matokeo ya Kituoni yatajazwa kwenye Fomu za Matokeo Na. 21B kwa Ubunge na Fomu Na. 21C kwa Udiwani.

(viii) Fomu Na. 21B ya Matokeo ya Ubunge Kituoni na Fomu Na. 21C ya matokeo ya Diwani Kituoni zitatiwa saini na Msimamizi wa Kituo/Msimamizi Msaidizi wa Kituo, Mawakala wa Vyama au Mgombea aliyepo Kituoni. Nakala moja watapewa Mawakala/Mgombea na nakala nyingine itabandikwa nje ya Kituo cha Kuhesabia kura.

(ix) Msimamizi wa Kituo/Msimamizi Msaidizi wa Kituo atapeleka Fomu za Matokeo ya Uchaguzi na vifaa vingine vilivyotumika kwenye zoezi la Upigaji Kura kwa Msimamizi wa Uchaguzi/Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

(x) Wakala wa kila Chama cha Siasa na mlinzi wa Kituo watakaokuwa Kituoni ambapo msafara unapoanzia wataruhusiwa kusindikiza msafara wa kupeleka matokeo ya

Uchaguzi kwenda kwa Msimamizi wa Uchaguzi/Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi wa Kata. Kwa upande wa Tanzania Bara na kwa Msimamizi wa Uchaguzi/Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi wa Jimbo la Dimani kwa upande wa Zanzibar.

(xi) Matokeo yote yakishapokelewa na Msimamizi wa Uchaguzi kwa upande wa Uchaguzi wa Ubunge na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kwa upande wa Uchaguzi wa Udiwani, yatajumlishwa mbele ya Mawakala na wote wanaoruhusiwa kuingia kwenye vituo vya Kujumlishia Kura.

(xii) Kama ilivyokuwa wakati wa Kuhesabu Kura, baada ya Ujumlishaji kukamilika matokeo ya Ubunge ngazi ya Jimbo yatajazwa katika Fomu Na. 24B na yale ya Diwani katika Kata yatajazwa katika Fomu Na. 24C. Fomu za Matokeo

hayo zitatiwa saini na Msimamizi wa Uchaguzi na Mawakala watakaokuwepo.

Mawakala watapewa Nakala za Fomu za Matokeo na Nakala moja itawekwa mahali pa wazi nje ya Kituo cha Kujumlisha Kura.

Ndugu Wananchi;

Pamoja na kuwakumbusha yanayopaswa kufanywa siku ya Uchaguzi Tume pia inapenda kusisitiza mambo muhimu yafuatayo:-

i. Mwisho wa Kampeni ni leo saa 12:00 jioni, Vyama, Wagombea na mashabiki baada ya saa 12 jioni wasifanye kampeni za aina yoyote ikiwa ni pamoja na kutumia alama zozote zinazoashiria Kampeni kama vile bendera, mavazi n.k.

ii. Mawakala wa Vyama vya Siasa wanaruhusiwa kuwepo Vituoni kwa mujibu wa Sheria na Kanuni, Wakala asiyekuwa na barua ya utambulisho kutoka kwa Msimamizi wa Uchaguzi

na ambaye hatakula kiapo cha kutunza siri hataruhusiwa kuingia katika Kituo cha Kupigia, Kuhesabia na Kujumlishia Kura.

iii. Vyama vyote vya Siasa vinavyoshiriki katika Uchaguzi vinatakiwa kuhakikisha kwamba vinaweka Mawakala katika vituo vyote vya Kupigia Kura na Kujumlishia Kura. Mawakala hao watatakiwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa.

iv. Kwa kuzingatia Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2015 yaliyokubaliwa na Vyama vyote vya Siasa, Wapiga Kura wanatakiwa kuondoka Vituoni mara baada ya kupiga kura ili kuendelea na shughuli zao. Vyama vya Siasa vimeweka Mawakala vituoni ambao watalinda maslahi ya Vyama husika na Wagombea wao.

v. Mpiga Kura atapiga Kura kwenye Kituo alichopigia Kura wakati wa Uchaguzi Mkuu wa 2015.

vi. Watu waliotajwa kwenye Sheria ya Uchaguzi ndiyo pekee wanaoruhusiwa kuingia kwenye Vituo vya Kupigia, Kuhesabia na Kujumlishia Kura.

vii. Mpiga Kura mwenye Ulemavu wa kutoona ataruhusiwa kuja kituoni na mtu atakayemchagua mwenyewe.

viii. Ni kosa la jinai Mpiga Kura Kupiga Kura zaidi ya mara moja.

ix. Mwenye mamlaka ya kumtangaza Mshindi ngazi ya Ubunge ni Msimamizi wa Uchaguzi na kwa ngazi ya Udiwani mwenye mamlaka ya kufanya hivyo ni Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

Ndugu Wananchi;

Kwa kumalizia, Tume inawasihi tena Wapiga Kura wote wanaoishi kwenye maeneo ya Uchaguzi Mdogo kujitokeza kwa wingi Kupiga Kura ili kuwachagua Viongozi mnaowataka wawaongoze kwa miaka mitatu ijayo.

Tume inapenda kuwahakikishia Wananchi wote kwamba, kutakuwa na ulinzi wa kutosha katika Vituo vya Kupigia Kura.

Ni matumaini ya Tume kuwa hali ya **Amani na Utulivu** ambayo imekuwepo hadi sasa na kama ilivyokuwa katika Chaguzi zilizopita itaendelea kudumishwa ili kuhakikisha Uchaguzi unafanyika kwa Utulivu na Amani kwa Ustawi wa Taifa letu.

Kila Mwananchi, Viongozi wa Dini na Vyama vya Siasa tushirikiane wote ili kuhakikisha kuwa viashiria vya kuvunjika kwa Amani na Utulivu vinaepukwa ili kuhakikisha Uchaguzi utakaofanyika unakuwa Huru, Wazi na wa Haki.

KUMBUKA, KUPIGA KURA NI HAKI YAKO YA MSINGI KWA MUSTAKABALI WAKO NA WA NCHI YAKO.

NENDA KAPIGE KURA.

MUNGU IBARIKI AFRIKA, MUNGU IBARIKI TANZANIA.

Ahsanteni kwa kunisikiliza.